



## Kwa hakika Mwenyezi Mungu atamchagua mtu mmoja katika umma wangu mbele ya mkusanyiko wa watu siku ya Kiyama

Imepokelewa kutoka kwa Abdullah bin Amrou binil Aaswi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake- "Kwa hakika Mwenyezi Mungu atamchagua mtu mmoja katika umma wangu mbele ya mkusanyiko wa watu siku ya Kiyama basi atamkunjulia mafaili tisini na tisa, na kila faili moja lina ukubwa sawa na upeo wa macho yanapoishia kuona, kisha atasema: Je unapingamizi katika haya yaliyopo ndani ya mafaili haya?, je waandishi wangu wenye kuhifadhi yenye kuandikwa wamekudhulumu? basi atajibu: "Hapana ewe Mola wangu, hawakunidhulumu": Basi atamwambia: Je unalakujitetea? Basi atasema: "Hapana ewe Mola wangu", atasema: Hakika wewe unayo matendo mema kwetu, na kwa hakika hautodhulumiwa chochote leo hii, basi atatolewa kadi iliyoandikwa Ash-hadu An-laa Ilaaha illa Ilaahu wa Ash-hadu Anna Muhammadan Abduhuu wa Rasuuluhu, hivyo atasema: Ewe Mola wangu ni kadi gani hii na ni faili gani hili? Basi atasema: Kwa hakika wewe hutodhulumiwa", Mtume akasema: Basi yatawekwa mafaili katika kipimo na kadi itawekwa upande wapili wa kipimo, basi ukawa mwepesi ule upande uliowekwa mafaili, na ukawa mzito ule upande uliowekwa kadi, na haiwezekani kitu chochote kuwa kizito kuliko neno la Tauhidi ambalo ni Laa Ilaaha illa Ilaah Muhammadan Rasuulullah."

[Sahih]

Alitoa habari Mtume -Rehema na mani ziwe juu yake- kuwa Mwenyezi Mungu atamchagua mtu katika umma wake kwenye kundi la watu siku ya Kiyama atamuita ili amuhesabu, basi atamtotea mafaili tisini na tisa na mafaili hayo ni ya matendo yake mabaya ambayo alikuwa akiyafanya Duniani, na urefu wa kila faili ni mfano wa upeo wa macho, Kisha Mwenyezi Mungu atamwambia mtu huyu: Je unapinga chochote katika haya yaliyoandikwa katika mafaili? Je Malaika wangu wenye kuhifadhi wanayoandika wamekudhulumu? Basi atasema mtu yule: Hapana ewe Mola wangu. Basi Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: Je una chochote cha kujitetea nacho katika matendo yako uliyoyatanguliza miongoni mwa matendo ya Duniani?katika matendo uliyoyafanya kwa kusahau au kwa kukosea au kwa kutojua, Basi atasema mtu yule: Hapana ewe Mola wangu sina chochote cha kujitetea nacho. Basi Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: Si hivyo, kwa hakika wewe una mambo yaliyoandikwa kwetu sisi, na kwa hakika wewe hutodhulumiwa leo hii. Akasema: Basi itatolewa kadi iliyoandikwa ndani yake: Ash-hadu An-laa ilaaha illa Ilaah wa Ash-hadu Anna Muhammadan Ab-duhuu wa Rasuuluhu. Basi atasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Angalia Mizani yako. Basi atasema mtu yule hali ya kuona ajabu: Ewe Mola wangu! ni uzito wanini huu wa kikadi kidogo

pamoja na kupimwa na mafaili yote haya? Basi atasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: hautadhulumiwa leo hii. Akasema: Basi mafaili yatawekwa katika sehemu ya kupimia, na Kadi kwenye sehemu nyingine ya kupimia; Hivyo basi ukawa mwepesi upande wa kupimia palipo na Mafaili na ukawa mzito upande wa kupimia palipo na Kadi, hivyo basi Mwenyezi Mungu akamsamehe.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/65033>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

